# Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

## TUMEITWA ILI TUWE WANAFUNZI

Yesu alipokuwa akitembea kando kando ya ziwa la Galilaya aliwaona ndugu wawili, Petro na Andrea, wakishusha nyavu zao ziwani. Ndipo Yesu akawaita na kuwaambia, “Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu.” Mara moja wakaacha nyavu zao na kumfuata (Mathayo 4:18-20).

Hata leo Yesu angali awaita watu wamfuate ili wawe wanafunzi wake. Mtu kuwa mwanafunzi wa Yesu ni zaidi ya kumkiri Kristo au kujiunga na ushirika wa kidini. Maana ya uanafunzi ni mtu kubadilisha mtindo wake wa maisha. Ni mtu kutoa maisha yake ili kufuata malengo na kusudi la Kristo—kuishi kama Yesu, kudumisha amri zake, na kufanya maamuzi ya maisha yake kwa kulingana na mafundisho ya Kristo. Mwanafunzi wa Kristo hana budi kuacha maisha yake ya kibinafsi, kama vile ambavyo Petro na Andrea waliacha nyavu zao ili kumfuata Bwana.



Maisha ya mwanafunzi wa kweli wa Kristo hayasukumwi na upendo wa ulimwengu, au utajiri na anasa za kilimwengu, bali huwa na msukumo unaotokana na mtu huyo kupenda sana mambo ya Mungu. Malengo ya mtu kama huyo, matamanio ya moyo wake, mipango yake, na anayotaka kufanya hulingana na malengo yake Kristo.

Yesu alitoa mawaidha kabambe ya maana kamili ya mtu kuwa mwanafunzi. Katika Mathayo 16:24-25 alisema yafuatayo, “Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate.” Maana ya mtu kuwa mwanafunzi ni yeye kujinyima mambo ya ulimwengu huu, na badala yake kumfuata Yesu na njia zake bila kujali gharama atakayolipa. “Basi, kadhalika kila mmoja wenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu” (Luka 14:33).

Hakuna nafasi kwa wanafunzi wenye mioyo vuguvugu. Inambidi mtu kujitoa na kukabidhi maisha yake kwa Kristo ili awe mwanafunzi wake. Petro na Andrea hawakubeba nyavu zao na kuzileta kwa Bwana alipowaita; iliwabidi waaachane nazo. Je, wewe uko tayari kuacha njia zako na kumfuata Kristo? Je, wewe ni mwanafunzi wa Yesu? Je, watu wakiangalia tunda la maisha yako wanaweza kuona mfano wake Kristo.

Mwanzoni Yesu aliwaita wanaume kumi na wawili ili wamfuate na kuwa wanafunzi wake. Isipokuwa Yuda Iskariote, wanafunzi hao wengine kumi na mmoja walitoa maisha yao mhanga kwa ajili ya malengo ya Kristo. Wito wao ulikuwa ni wa kuwasaidia watu na kueneza injili. Kumi kati ya hao waliteswa na kuuawa kwa ajili ya imani yao. Wanafunzi hawa wa mwanzo wa Kristo walikuwa na ujasiri mwingi na wanahitaji kutupa changamoto hata leo na kutuhimiza tuitikie wito wa Kristo na kuacha YOTE ili tuwe wanafunzi wake Yesu. ■

> “Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate” Mathayo 16:24-25.”


Tumeitwa Ili Tuwe Wanafunzi 1

Tahariri 2

Simoni (Petro) 3

Andrea, Yakobo, Yohana, Filipo 4-5

Bartholomayo, Tomaso, Mathayo, Yakobo, Thadayo 6-7

Simoni Mkananayo
Yuda Iscariote 8

# TAHARIRI



*Kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii ...* — Waebrania 12:1

Toleo hili la Ukweli wa Injili ni tofauti kwa kiwango fulani na matoleo ya hapo awali ya jarida hili, kwa maana hili halina sehemu ya Mafunzo ya Biblia na makala yanayohusiana na mafunzo hayo ya Biblia. Badala yake nimepokeo himizo la kushiriki nanyi muhtasari wa maisha na vifo vya kila moja wa wanafunzi kumi na wawili wa Yesu. Maisha yao ya kimisheni na kujitolea kwao ni mambo ambayo yaliathiri sana mianzo ya kanisa kwa kiwango kikubwa. Baadhi ya wanafunzi hao walikuwa nguzo muhimu ya uandishi wa maandiko matakatifu kulingana na vile walivuviwa na Mungu.

Maisha yao ya kujitolea yangali yanatuonyesha, hata baada ya miaka elfu mbili, maana ya mtu kuwa mwanafunzi wa Yesu. Wengi wao walikuwa tayari kuteseka na kufa badala ya kuikana imani yao kwa Kristo. Leo hii Wakristo wengi hushindana na mambo madogo sana yakilinganishwa na changamoto zilizowapata wanafunzi hao wa mwanzoni. Hebu basi Bwana atusaidie ili tuitikie wito wa kuwa wanafunzi wa Kristo ili tufuate mapenzi ya Mungu kwa dhati. Kuna haja ya sisi kuwa na mwelekeo wa kujitolea zaidi, na kuweka wakfu maisha yetu kwa Yesu. Wengi wetu humshikilia Kristo kwa mkono mmoja ilhali ule mwingine umeshikilia ulimwengu. HEBU BASI TUACHILIE ulimwengu na kuyakana yote kwa ajili ya kumfuata Yesu!

Ombi langu ni kwamba Mungu atakupatia himizo na changamoto ya kujito zaidi kwa Yesu Kristo unaposoma hadithi hizi kuhusu wanafunzi wale "KUMI NA WAWILI."

Michael W. Smith

Januari, 2025



## Wanafunzi wa Yesu

- Simoni (Petro)
- Andrea (ndugu yake Petro)
- Yakobo (mwana wa Zebedayo)
- Yohana (ndugu ya Yakobo)
- Filipo
- Bartholomayo (Nathanaeli)
- Tomaso
- Mathayo (Lawi)
- Yakobo (mwana wa Alfayo)
- Thadayo (Lebausi, Yuda)
- Simoni Mkananayo/Zelote
- Yuda Iskariote

[Mathayo 10:2-4; Marko 3:14-19; Luka 6:13-16]



Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya *www.thegospeltruth.org* na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.
—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@the gospeltruth.org

# Wanafunzi Kumi na Wawili

Habari ifuatayo, ambayo ni ya wasifu, imechimbuliwa kutoka machimbuko mbalimbali. Lakini kando ya Maandiko, kuna ushahidi kidogo sana wa habari ambazo tumeandika hapa. Wakati mwingine maelezo yaliyoko hapa yametolewa kutoka kwa maandishi ya kihistoria ambayo yanatofautiana, na pia kutokana na habari za mapokezi ambazo huchora taswira ya maisha na vifo vya watu hawa. Historia ya wanafunzi kumi na wawili ni jambo linalotupatia uvuvio mwingi, lakini pia ni jambo ambalo linatupatia changamoto. Basi ni muhimu kwetu kutambua kwamba Agano Jipya ndilo linatupatia habari nyingi zaidi kuhusu wasifu wa mtu ambaye ni mhusika mkuu kabisa katika Ukristo—Yesu Kristo, Mwokozi na Mkombozi wetu. (Michoro yote iliyochorwa hapa ni kwa ajili ya kusaidia katika maelelezo tu).

## PETRO

### MWAMBA, KIONGOZI WA KIDINI MWENYE MISUKUMO MIKUU



Mtume Petro, mwanzoni akijulikana kama Simoni, alikuwa mvuvi kutoka Bethsaida, hapo kando ya Ziwa la Galilaya. Baadaye Petro aliishi Kapernaumu pamoja na mke wake, pia wakiwa na ndugu yake Andrea. Petro alijulikana kama mtu shujaa ambaye alikuwa na misukumo aliyozaliwa nayo, lakini akafanyika kuwa mmoja wa wanafunzi wa karibu sana wa Yesu, baada ya Yesu kumwita ili amfuate. Yesu ndiye alimpa jina "Petro" (yaani "mwamba"), jina ambalo baadaye lilielezea sifa za kiroho za mtume huyu. Yeye pia anajulikana kama "Kefa" (Yohana 1:42; 1 Wakorintho 1:12; 3:22; 15:5; Wagalatia 2:9), ambalo ni neno la Kisiriaki lenye maana ya  mwamba au jiwe.

Petro alikuwa mmoja wa wandani wa Yesu, na alikuwepo katika nyakati muhimu sana za Yesu, kama vile Kugeuzwa kwake (Mathayo 17:1-8) na mateso yake kwenye Shamba la Gethsemane (Mathayo 26:36-37). Ingawa yeye alikuwa mtu mwenye imani kubwa, safari ya Ukristo ya Petro ilijaa ujasiri uliochanganyika na udhaifu.

Tendo la Petro ambalo linajulikana sana ni lile la kutembea juu ya maji kumwendea Yesu, lakini akaanza kuzama majini wakati alipoanza kuwa na shaka (Mathayio 14:29-30). Na wakati Yesu alipofanyiwa mashtaka, Petro alimkana mara tatu kutokana na woga. Baadaye Petro alitubu na baada ya Yesu kufufuka Yeye alimrudisha Petro wadhifa wake na kumpatia wajibu wa "kulisha wanakondoo wake" (Yohana 21:15-17).

Baada ya Yesu kupaa kurudi mbinguni Petro aliibuka na kuwa kiongozi muhimu wa kanisa la kwanza, na uongozi wake ukawa na sifa ya utimamu kama mwamba. Yeye hasa alihudumu kati ya waumini wa Kiyahudi huko Yerusalemu. Na ni yeye alifanya mahubiri ya mwanzo katika Siku ya Pentekote, wakati ambapo watu 3,000 walitubu na kuokoka (Matendo 2). Petro alifanya miujiza na kungoza kanisa la Yerusalemu, na pia akatetea kuingizwa kwa watu wa Mataifa katika imani ya Kristo (Matendo 10). Habari za mapokezi zinasema kwamba baadaye Petro alisafiri na kwenda Antiokia, na mwishowe kufika Roma, mahali ambapo aliendelea na huduma yake hata ingawa kulikuwa na mateso dhidi ya Wakristo.

Inaaminiwa kwamba Petro ndiye aliyeandika vitabu viwili vya Agano Jipya, Petro wa Kwanza na wa Pili, ambavyo vinawahimiza waumini kuvumilia mateso na kuzidi kuwa waaminifu. Ni jambo la kuzingatiwa kwamba Yohana Marko ndiye aliandika kitabu ya Marko, ambacho msingi wake ni mambo ambayo yeye alijifunza kutokana na ushuhuda wa Petro, ushuhuda wa kujionea kwa macho. Takriban miaka ya 64-68 baada ya kuzaliwa kwa Yesu, Petro aliuawa kwa ajili ya imani yake huko Roma katika utawala wa Mfalme Nero. Mapokezi yanasema kwamba yeye alisulubiwa kichwa chini miguu juu kutokana na ombi lake kwamba hakujihisi kustahili kufa kwa njia iliyolingana na ile ya Yesu. Maisha yake ni mfano bora wa mtu ambaye amegeuzwa kutoka kuwa mwanafunzi mwoga, hadi anakuwa kiongozi jasiri. Yeye anakumbukwa kama nguzo ya imani na "mwamba" wa kanisa." ■

# ANDREA

## MPATANISHI, MTU MWENYE KULETA WATU KWA YESU



Andrea, ndugu yake Petro, kitaaluma alikuwa mvuvi. Yeye alizaliwa Bethsaida, ambacho kilikuwa ni kijiji cha wavuvi kando kando ya Ziwa la Galilaya. Kabla ya kuwa mwanafunzi wa Yesu, Andrea alikuwa mfuasi wa Yohana Mbatizaji, na humo ndipo alipatana na Yesu kwa mara ya kwanza. Baaa ya ushuhuda wa Yohana Mbatizaji kwamba Yesu alikuwa Mwanakondoo wa Mungu, Andrea akafanyika kuwa mmoja wa wanafunzi wa mwanzo wa Kristo (Yohana 1:35-40). Tendo lake la kwanza baada ya kuanza kumfuata Yesu, lilikuwa ni kumleta ndugu yake Petro kwa Yesu, jambo ambalo lilionyesha shauku yake ya umisheni ambayo ilikuwa ndani yake.

Baada ya kuitwa na Yesu, Andrea alitembea naye na kushiriki katika matukio muhimu kwenye huduma ya Yesu. Yeye anatambulika kwa wajibu wake katika tukio la kulishwa kwa watu 5,000, wakati ambapo ni yeye alimtambua kijane aliyekuwa na mikate mitano na samaki wawili (Yohana 6:8-9). Na baada ya Yesu kufufuka, Andrea alifanyika kuwa kiongozi muhimu katika kanisa la kwanza, hasa kati ya makundi ya waumini wa Kiyahudi.

Mapokezi yanasema kwamba Andrea alihubiri katika sehemu tofauti tofauti, ikiwemo Yudea, Samaria, na pia sehemu zilizokaribia Ziwa Nyeusi, pamoja na sehemu za nchi za kisasa zinazojulikana kama Ugiriki na Uturuki. Kulingana na maadishi mengine inaonekana kwamba yeye alisafiri hadi Scythia (sehemu a Ukraine na Urusi) akihubiri Injili kwa watu wa Mataifa na kuanzisha makundi ya Kikristo.

Kuuawa kwa Andrea kwa sababu ya imani yake yaaminika kulifanyaka takriban miaka ya 60-70 baada ya Yesu kuzaliwa, huko Patras, nchini Ugiriki. Mke wa gavana alikuwa ameponywa kimuujiza na akaamua kuokoka, jambo ambalo lilimkasirisha mumewe sana, na ndiposa akamhukumu Andrea kuuawa kwa kusulubiwa. Kutokana na ombi lake, Andrea alisulubishwa katika msalabwa uliotengenezwa kwa mfano wa X, kwa sababu hakujihisi kwamba alistahili kufa kwa mfano mmoja na bwana wake Yesu. Alipokuwa hapo msalabani Andrea aliwahubiria watu kwa siku mbili mfululizo.

Urithi wa Andrea kama muinjilisti na kujitolea kwake kueneza ujumbe wa Yesu ni mambo muhimu. Maisha yake ni kielelezo kizuri cha roho ya uanafunzi na umuhimu wa sisi kuwafikia wengine. Yeye alikuwa na athari bora katika kanisa za kuwa chanzo cha watu wengi kumfuata Kristo. ■

# FILIPO

## MTAFUTI WA UKWELI, MISHENARI MWENYE VITENDO HALISI



Filipo alikuwa mkazi wa Bethasaida, mji ule ule ambao Petro na Andrea walitoka (Yohana 1:44). Ni muhimu kukumbuka kwamba Filipo anayezungumziwa hapa sio yule Filipo muinjilisti (Matendo 6:5). Filipo alijulikana kutokana na shauku yake ya kutaka kujua mambo sana, na alikuwa mmoja wa wanafunzi wa kwanza wa Yesu. Baada ya kukutana na Yesu, mara moja Filipo alimtambua Yesu kama yule ambaye alitimiza unabii wote. Ndiposa akamleta rafiki yake Nathanaeli (ambaye pia alijulikana kama Bartholomayo) ili wakutane na Yesu, huku akisema, "Tumemwona yeye aliyeandikiwa na Musa katika torati, na manabii" (Yohana 1:45). Utangulizi huu unaonyesha jinsi Filipo alivyokuwa na moyo wa kushiriki imani yake na kuwaleta watu wengine kwa Kristo.

Filipo ametajwa mara kadhaa katika vitabu vya Injili, mara nyingi akiuliza maswali ambayo yanaashiria shauku yake ya kutaka kuelewa zaidi mafundisho ya Yesu. Katika Yohana 6:5-7 Filipo anaelezea tashwishi zake za kibinadamu kuhusu uwezekano wa kuwalisha watu 5,000, jambo ambalo linaonyesha hali yake ya kuchukulia mambo kwa uhalisi wake. Baadaye alimwomba Yesu awaonyeshe Baba, jambo ambalo lilimfanya Yesu kueleza umoja wake na Baba (Yohana 14:8-9).

Baada ya Yesu kupaa na kurudi mbinguni Filipo alichukua jukumu la kimishenari, na mapokezi ya Kanisa la Mwanzo yanaashiria kwamba yeye alihubiri katika sehemu za Samaria, Siria, na Frijia (ambayo sasa inajulikana kama Uturuki), na huenda pia alihubiri katika nchi ya Ugiriki. Pia anahusishwa na uenezaji wa Injili katika sehemu ambazo baadaye zilifanyika kuwa ngome za Kanisa la mwanzo.

Kuna nakala kadhaa za vile Filipo aliuawa kwa ajili ya imani yake. Kulingana na wanahistoria kadhaa, Filipo aliuawa katika mji wa Hierapolisi huko Frigia (Uturuki) ambako alinyongwa (kichwa chini miguu juu) msalabani takriban mwaka wa 80 baada ya kuzaliwa kwake Yesu. Nakala zingine zinasema kwamba alikuwa akihubiri Kaskazini mwa Afrika, ambako aliuawa kwa kupigwa mawe au kunyongwa kwa kupitia vifundo vyake vya miguu.

Athari nzuri za Filipo zinapatikana katika nyanja za kimisheni na kujitolea kwake ili kueneza Injili katika sehemu tofauti tofauti. Hadithi yake inadhihirisha mchanganyiko wa kufuatilia uhalisi wa mambo na pia mtu kuwa na imani dhabiti. ■

# YOHANA

## MWANAFUNZI ALIYEPENDWA, MWALIMU WA UPENDO NA UKWELI



Yohana, ambaye mara nyingi anajulikana kama “mwanafunzi aliyependwa,” alikuwa ndugu yake Yakobo, mwana wa Zebedayo. Yeye alizaliwa huko Bethsaida, kijiji cha wavuvi, kilichokuwa kando kando ya Ziwa la Galilaya, lakini baadaye alihama na kuishi Kapernaumu. Kabla ya kumfuata Yesu, Yohana alifanya kazi kama mvuvi pamoja na baba na ndugu yake. Ndiposa Yesu akamwita pamoja na ndugu yake (Yakobo) ili wawe wanafunzi wake, na muda si muda wao wakawa sehemu ya wandani wa Yesu. Wawili hao walishuhudia matukio makuu katika huduma ya Yesu, ikiwa ni pamoja na Kubadilishwa kwa Yesu. Tunahitaji kuzingatia kwamba Yohana ndiye mtume pekee ambaye alibaki miguuni pa Yesu wakati aliposulubiwa, jambo lililoonyesha kujitolea na upendo wake kwa Yesu. Katika miaka ya mwanzoni Yohana alionekana kuwa mtu wa kujitakia makuu, na aliyekuwa tayari kuwasukuma wengine kando, kama wakati alipomzuia mtu fulani asitoe pepo kwa jina la Yesu (Marko 9:38-41), na wakati alitaka kuita moto kutoka mbinguni (Luka 9:51-54); na zaidi, wakati aling’ang’ana ili awe mkuu zaidi (Mathayo 20:20-24). Baadaye Yohana alikomaa na kufanyika kuwa mtu mwenye upendo na unyenyekevu mwingi, na hata Yesu akampatia kazi ya utunzi wa mama yake (Yohana 19:25-27).

Baada ya Yesu kufufuka na kupaa mbinguni, Yohana alichukua jukumu muhimu katika kanisa la mwanzo, hasa huko Yerusalemu. Yeye alikuwa nguzo muhimu sana ya uenezaji wa Injili kati ya Wayahudi, na baadaye kati ya watu wa Mataifa. Na inaaminika kwamba Yohana pia alihubiri huko Asia Ndogo, hasa Efeso, mahali ambapo alifanyika kuwa kiongozi muhimu katika jamii ya Wakristo.

Yohana alikamatwa huko Efeso na kutupwa katika pipa kubwa la mafuta yaliyokuwa yakichemka; lakini Mungu alimwokoa kimuujiza. Ndiposa baadaye akahamishwa na kupelekwa kwenye kisiwa cha Patmo na Warumi, mahali ambapo alipata maono ya Yesu Kristo na kundika kitabu cha unabii cha Ufunuo wa Yohana.

Yohana pia alijulikana kwa majina mengine: Yohana wa Patmo, Yohana Mwinjilisti, Yohana Mzee (wa Kanisa), na Presbita Yohana. Yeye amesemwa kwamba ndiye aliandika vitabu vitano vya Agano Jipya: Injili ya Yohana, nyaraka tatu za Yohana (wa 1, wa 2 na wa 3), na pia kitabu cha Ufunuo. Maandishi yake yanatilia mkazo masuala ya upendo, imani, na uungu wa Kristo, na yamejaa mielekeo kabambe kwa maswala ya kithiolojia.

Habari za mapokezi zinasema kwamba Yohana aliishi sana mpaka akawa kizee chenye miaka mingi, na huenda ikawa alikufa huko Efeso, na inadhaniwa kwamba alikufa mwakani 100 baada ya kuzaliwa kwa Yesu. Inasemekana kwamba yeye alikufa kutokana na magonjwa ya uzeeni, jambo ambalo ni tofauti na wengi wa mitume, ambao waliuawa kwa ajili ya imani yao. Urithi wake kama mwanathiolojia na mwinjilisti ni mambo ambayo yameathiri Ukristo pakubwa kwa uzuri, na maisha yake huchukuliwa kuwa mfano bora wa uaminifu na mtu kujitolea kwa Yesu. ■

# YAKOBO

## MWANA WA NGURUMO, MFIA IMANI JASIRI



Yakobo mwana wa Zebedayo na Salome, alikuwa ndugu yake Yohana, na wakati mwingi alijulikana kama “Yakobo Mkuu,” hii ikiwa ni kumtofautisha na Yakobo mwana wa Alfayo. Yeye alikuwa mvuvi kutoka Bethsaida, Galilaya. Wakiwa na ndugu yake Yohana wao walifanya kazi katika biashara ya uvuvi na baba yao, kabla ya Yesu kuwaita ili wamfuate (Mathayo 4:21-22). Yakobo alijulikana kwa sifa zake za maumbile za kuwa mtu mwenye ari, ndiposa Yesu akampatia jina pamoja na ndugu yake Yohana na kuwaita “Wana wa Ngurumo” (Marko 3:17). Mara tu Yakobo alipoitwa alifanyika mmoja wa wandani wake Yesu, akiwemo pia Petro na Yohana. Yeye alikuwemo katika matukio mengi makuu ya maisha yake Yesu. Yakobo alikuwa chanda na pete na ndugu yake Yohana, kamwe hawangeachana.

Yakobo alikuwa mhusika muhimu kati ya jamii ya Wakristo wa kanisa la kwanza, hata ingawa ni machache sana yaliyoandikwa kuhusu huduma yake. Huduma ya Yakobo ilizingatia hasa kuhubiria vikundi vya Wayahudi huko Yerusalemu na Yudea. Tamaduni za mapokezi zinasema kwamba Yakobo ndiye alipeleka Injili huko Uhispania, hata ingawa hakuna maandishi halisi yanayosema hivyo. Utu wake wenye ushupavu mwingi na shauku yake ya kueneza ujumbe wa Yesu ulimfanya kuwa shahidi jasiri wa Injili. Lakini ari hii pia ilimfanya Mfalme Herode Agripa I kumlenga, na mfalme huyo alikuwa mwenye mtazamo kwamba athari za kanisa zilikuwa ni tishio kubwa la kisiasa kwake. Ndiposa hapo karibu mwaka wa 44 baada ya kuzaliwa kwake Yesu, Herode aliamuru Yakobo kuuawa kwa kukatwa upanga (Matendo 12:1-2). Tendo hili la Yakobo kufa kwa ajili ya imani lilikuwa ishara ya mambo kubadilika katika kanisa la kwanza, kwa maana yeye ndiye alikuwa mtume wa kwanza kuweka muhuri ushuhuda wake kwa kutoa maisha yake.

Kama mmoja wa wanafunzi wa karibu sana wa Yesu, maisha ya Yakobo yalidhihirisha imani ambayo haitingisiki na maisha ya kujitolea, jambo ambalo lilimfanya kuwa mtu shupavu kati ya mitume. Ujasiri wake na kujitolea kwake kwa Yesu mpaka mwisho wa maisha yake ni jambo ambalo limewapatia Wakristo motisha katika imani yao kwa karne nyingi, kwa sababu maisha yake yalikuwa dhihirisho la gharama na kujitolea kwa mtu kama mfuasi wa Kristo. ■

## BARTHOLOMAYO (NATHANAELI)

### MWISRAELI WA KWELI ASIYE NA HILA



Bartholomayo alizaliwa Kana ya Galilaya (Yohana 12:2), mahali ambapo huenda Yesu alifanya muujiza wake wa kwanza. Bartholomayo hasa anajulikana kama Nathanaeli, na aliletwa kwa Yesu na Filipo. Mwanzoni Nathanaeli alikuwa na tashwishi zake, ndiiposa akauliza, “Laweza neno jema kutoka Nazareti?” (Yohana 1:46), lakini baada ya kukutana na Yesu, na kusikia kwamba Yesu alimjua kama “Mwisraeli kweli kweli, hamna hila ndani yake” (Yohana 1:47) Nathanaeli aliweza kuamini mara moja. Nafasi hiyo ya kutafuta ukweli kwa njia halisi, na imani yake kuchipuka papo hapo, ilikuwa mwanzo wa Bartholomayo kujitoa kwake Yesu kwa njia ya uaminifu.

Baada ya Yesu kupaa mbinguni, Bartholomayo alisambaza Injili katika sehemu zingine kama vile India, Mesopotamia (Iraq), Uajemi (Iran), Lycaonia (Uturuki), Misri, Armenia, na hata maandishi mengine yanasema aliweza kufika Ethiopia na huko Rasi ya Uarabuni. Pia inasemekana kwamba huko India aliweza kuhubiri injili kwa kutumia lugha za mumo humo, aidha kwa njia ya ujumbe wake kutafsiriwa kwa lugha za huko, au kwa yeye kuweza kujifunza na kunena kwa lugha hizo.

Urithi wa Bartholomayo unakumbukwa sana hasa huko Armenia ambako alishiriki jukumu muhimu ya kuwahubiria na kuokolewa kwa watu wengi, hata ingana yeye alipambana na pingamizi kubwa kutoka kwa makuhani wa sehemu hiyo wa kipagani. Kifo chake kilikuwa cha ukatili mkali kwa sababu inaaminika kwamba yeye alichipuliwa ngozi ya mwili huku akiwa hai, na pia kukatwa shingo katika nchi hiyo ya Armenia, hapo karibu mwaka wa 68 baada ya kuzaliwa kwake Kristo. Tukio hilo la kifo chake ni dhihirisho la imani yake isiyotingisika, hata wakati ikipambana na pingamizi kali. ■

## YUDA ISKARIOTE

### MSALITI



Yuda Iskariote alikuwa mtu mwenye sifa mbaya ya kumsaliti Yesu Kristo. Wasomi wengine wanasema kwamba neno Iskariote linamaanisha “mtu wa kutoka Keriothi,” ambao ulikuwa ni mji huko Yudea. Kama huu ni ukweli, basi hii inamaanisha kwamba yeye alikuwa ndiye mtume pekee wa kutoka Yudea, na pia kumaanisha kwamba alikuwa mtu wa “nje.” Katika Biblia Yuda anaonyeshwa kuwa ndiye alikuwa mweka hazina wa kikundi, lakini pia anaonyeshwa kuwa alikuwa ni mwizi, ambaye alikuwa akiibia mkoba wa kikundi (Yohana 12:6). Hata baada ya kushuhudia miujiza yake Yesu, Yuda alijitoa kwa majaribu ya tamaa na kwa kuutii moyo wake uliokuwa umevunjika. Ndiposa akakubali kumsaliti Yesu kwa fedha thelathini, na akapanga jinsi Yesu angekamatwa katika Shamba la Gethsemane (Mathayo 26:14-16).

Baada ya Yesu kuhukumiwa, Yuda alijihisi majuto, ndipo akarudisha fedha zile kwa makuhani na kujitia kitanzi (Mathayo 27:3-5). Huu mwisho wake mbaya ulikuwa ni matokeo ya maamuzi yake, na unakutukumbusha haja ya sisi kukazana dhidi ya dhambi, na haja yetu ya kupata ukombozi kutoka kwa maisha ya dhambi. Maisha ya Yuda yanaonyesha kwamba mtu anaweza kutoa wakati wake kwa Yesu bila yeye kumpatia moyo wake. ■

## YAKOBO (MWANA WA ALFAYO)

### MWANAFUNZI MWAMINIFU, LAKINI AMBAYE HAKUJULIKANA SANA



Yakobo mwana wa Alfayo, mara nyingi akiitwa “Yakobo Ambaye Hakujulikana Sana,” au “Yakobo Kijana” kumtofautisha na Yakobo ndugu yake Yohana, ambaye alijulikana kama “Yakobo Mkuu.” Ni machache sana yameandikwa kuhusu Yakobo wa Alfayo katika Agano Jipya, lakini huenda ikawa alizaliwa Galilaya. Mapokezi mengine yananasema yeye alikuwa ndugu yake Mathayo, kwa maana wote wawili walijulikana kama “wana wa Alfayo,” hata ingawa jambo hili halina uhakika. Pia yeye hukanganywa na Yakobo Mwenye Haki, ambaye alikuwa ndugu au binamu yake Yesu.

Kwa sababu hakuna mengi yamesemwa katika Agano Jipya kumhusu Yakobo wa Alfayo, mengi yanayojulikana yanatokana na mapokezi ya kanisa. Mapokezi mengine yanasema kwamba yeye alihubiri huko Yudea, na baadaye akapeleka umisheni wake Misri, ambako alisambaza Ukristo kati ya Wayahudi na jamii za kipagani.

Haijulikani vizuri jinsi Yakobo alifariki, kwa maana kuna mapokezi tofauti kuhusiana na swala hili. Klementi wa Alekisandria na waandishi wengine wanasema kwamba yeye alipigwa mawe na kuchapwa na kundi la watu hadi akafa hapo karibu mwaka wa 62 baada ya kuzaliwa kwake Yesu. Ilhali mapokezi mengine yanasema kwamba alisulubiwa au kuchapwa kwa rungu huko Misri. Lakini hata ingawa hakuna rekodi kamili ya kifo chake, yeye hukumbukwa kama mtume mwaminifu, lakini ambaye hakujulikana sana.

Hata ingawa Yakobo hakuandika kitabu chochote cha Biblia, urithi wake kama mfuasi timamu wa Yesu ni jambo ambalo linashangiliwa sana. Yeye ni kielelezo kizuri cha huduma ya kujitolea kwa njia ya unyenyekevu bila kufanya makelele mengi, na basi ni mwakilishi wa wanafunzi ambao wako tayari kueneza injili bila kutamani kutambulika sana. ■

# MATHAYO (LAWI)

## MKUSANYAJI USHURU, MWANDISHI WA MAFUNDISHO YA YESU



Mathayo, ambaye pia anajulikana kama Lawi, alikuwa mzaliwa wa Kapernaumu, mji uliokuwa kando ya Ziwa la Galilaya. Yeye alikuwa mkusanyaji ushuru kabla ya kuitwa kumfuata Yesu (Mathayo 9:9). Wakusanyaji ushuru walikuwa watu ambao sana sana hawakupendwa na jamii ya Wayahudi, kwa maana walionekana kushirikiana na mamlaka ya serikali ya Kirumi, na pia wakahushishwa na mambo ya kupenda hongo. Lakini Yesu alimwita Mathayo ili amfuate, na Mathayo akajitoa kwake mara moja na kuachana na kazi hiyo yake ya ukusanyaji ushuru ambayo ilikuwa na mapato mengi. Muda tu baada ya kuitwa Mathayo alifanya karamu kubwa kwa heshima ya Yesu, huku akiwaalika wakusanyaji ushuru wenzake wakiwa na wenye dhambi wengine. Hata ingawa jambo hili lilikashifiwa na Mafarisayo, ni jambo lililoonyesha moyo wa Mathayo uliokuwa na shukrani, pamoja na kujitolea kwake kwa Yesu Kristo (Mathayo 2:15-17).


Baada ya Yesu kupaa kwenda mbinguni Mathayo alijitwika jukumu la kuwa mishenari, na akaeneza injili, mwanzoni akifanya hivyo kati ya makundi ya Kiyahudi. Kulingana na mapokezi ya kanisa la kwanza, Mathayo alihubiri hasa kati ya Wayahudi, jambo ambalo linakubaliana na mafundisho na marejeleo ya unabii wa Kiyahudi yanayopatikana katika Injili hiyo yake ya Mathayo. Huenda pia ikawa kwamba kazi yake ya umishenari ilifika sehemu zingine, ikiwemo Ethiopia, na pengine hata sehemu za Parthia (Iran) na Siria.

Biblia haijanakili jinsi Mathayo alivyofariki, lakini mapokezi kadhaa yanaashiria kwamba yeye aliuawa kwa sababu ya imani yake. Mapokezi ambayo yanajulikana sana yanasema kwamba yeye aliuawa huko Ethiopia kwa kudungwa kisu. Mambo hayo hayajasemwa kinagaubaga, lakini mapokezi mengi yanakubaliana kwamba Mathayo aliifia imani yake kati ya miaka ya 60-70, baada ya kuzaliwa kwake Kristo.

Mathayo anajulikana zaidi kutokana na Injili ambaye inaitwa kwa jina lake, na ambayo iliandikwa ili kudumisha rekodi kamili ya maisha na mafundisho ya Yesu, hasa ikitilia umuhimu jinsi ambavyo Yesu alitimiza unabii wa Kiyahudi kuhusiana na swala la Masihi. Injili hii ambayo ni moja ya maandishi ya zamani sana ya Kikristo ni nguzo muhimu ya Agano Jipya, na inaonyesha kujitolea kwa Mathayo ili kuushiriki ujumbe wa Kristo. ■

# TOMASO

## MTU ALIYEKUWA NA SHAKA, NA AMBAYE ALIGEUZWA NA KUWA MUUMINI JASIRI



Tomaso, ambaye pia anajulikana kama "Tomaso Mwenye Shaka," anajulikana sana kwa vile alikuwa mwenye shaka hapo mwanzoni, wakati aliposikia kuhusu kufufuka kwa Yesu. Kama ilivyokuwa kweli kwa wengi wa wanafunzi, huenda ikawa Tomaso pia alizaliwa huko Galilaya. Neno lake la Kiebrania, Tomaso, linamaanisha "mapacha," na kwa lugha ya Kiyunani yeye pia anajulikana kama "Didimasi," jina ambalo lina maana hiyo hiyo. Hata ingawa hakuna mengi yanayojulikana kuhusu maisha yake ya mwanzoni, Tomaso ametajwa katika Injili zote nne, na anajulikana sana kwa ajili ya maumbile yake ya kiasili ya kutaka kuuliza maswali, na pia mwelekeo wake wa kupenda uhalisi wa mambo.

Katika Injili ya Yohana, Tomaso anaonekana hasa baada ya Yesu kufufuka, wakati aliposema waziwazi kwamba hataamini ufufuo huo kabla ya yeye kuona na kuguza majeraha yake (Yohana 20:24-29). Baadaye, wakati Yesu alipomtokea Tomasa na kumwalika aguze makovu yake, Tomasa alipaza sauti na kusema, "Bwana wangu na Mungu wangu," jambo ambalo lilionyesha imani yake. Tukio hili linaonyesha safari ya Tomasa kutoka kwa mtu aliyekuwa na tashwishi nyingi, hadi akawa mtu mwenye imani kubwa, na yeye ni mfano bora kwa watu ambao wana mashindano ya kuwa na imani timamu.

Kutoka kwa mapokezi ya kanisa inaonekana kwamba Tomasa alifanyika kuwa mishenari jasiri baada ya Yesu kupaa kwenda mbinguni. Inaaminika kwamba yeye alisafiri na kwenda sehemu za mashariki, na kueneza Injili katika sehemu za Parthia (Iran/Iraq). Yeye alikuwa ni mmoja wa mishenari mkakamavu sana kati ya wanafunzi wa Yesu, na alisafiri kwenda nchi nyingi za kigeni. Mwishowe akafika huko India takriban mwaka wa 52 baada ya kuzaliwa kwake Yesu. Mapokezi ya kale ya habari za Ukristo, hasa yale ya Wakristo wa huko Kerala, India, zinadai kwamba Tomaso ndiye alianzisha makundi ya Kikristo katika Pwani ya Malabar. Jamii hizi za Kihindi zingali zinamtambua Tomaso kama mwanzilishi wa imani yao.

Inasemekana kwamba Tomaso aliuawa kwa sababu ya imani mwakani 72 baada ya kuzaliwa kwake Kristo, katika sehemu ya Mylapore, sehemu ambayo kwa leo inajulikana kama Chennai, India. Kulingana na maandishi ya Kikristo, Tomaso alidungwa kwa mkuki ambao ulipitia moyoni mwake, akauawa kutokana na pingamizi alizopatana nazo kutoka kwa makundi ya kitamaduni ya kidini. Lakini urithi wake ungali wadumu kutokana na safari yake ya imani ambayo ilikuwa ya kuvutia sana, kutoka kuwa muumini mwenye shaka nyingi akaja kuwa mtu mwenye imani, na pia kupitia makundi ya Kikristo ya huko India. ■

# SIMONI (MKANANAYO/ZELOTE)

## MWANAMAPINDUZI ALIYEKUWA NA SHAUKU, AKAGEUKA NA KUWA MFUASI MWENYE BIDII



Simoni Zelote alijulikana pia kama Simoni Mwenye Bidii  au Simoni Mkananayo. Yeye huitwa "Zelote," jina ambalo linaonyesha uhusiano wake na vuguvugu la kisiasa la Kiyahudi ambalo lilitaka kung'oa Serikali ya Kirumi kutoka huko Yudea kwa njia yoyote ile, ikiwa ni pamoja na matumizi ya mabavu. Jambo hili linaonyesha kwamba Simoni alikuwa mtu mwenye ari kubwa kuhusu swala la utaifa wa Kiyahudi, na inawezkana kwamba yeye alikuwa mtu mwenye sifa za ukali.

Watafiti wengi wanaamini kwamba Simoni alizaliwa huko Galilaya, mahali walikotoka wengi wa mitume. Katika orodha ya mitume ambayo inapatikana katika vitabu vya Injili, Simoni wakati mwingi anaitwa "Mkananayo," jambo ambalo laweza kuashiria sehemu ambako alizaliwa, wala sio kabila lake; lakini pia inaweza kuwa jina hilo lilitokana na neno la Kiaramaiki la "qanana," kumaanisha "zelote."

Baada ya Yesu kufufuka Simoni alifanyika kuwa mwinjilisti hodari, na alifanya kazi ya kueneza injil katika sehemu tofauti tofauti. Mapokezi ya Kanisa la Mwanzo yanaashiria kwamba yeye alihubiri katika sehemu za Misri na Afrika Kaskazini, na pengine hata akafika Uigereza na Uajemi, ingawa nakala za habari hizo hazikubaliani, na pia hakuna rekodi timamu ya jambo hilo kihistoria.

Hamna habari kabambe na ya kuaminika kuhusiana na kifo cha Simoni, na hata habari ya mapokezi yanayohusu suala hili yanatofautiana. Habari zingine zinasema kwamba Simoni aliuawa kwa ajili ya imani yake hapo karibu miaka ya 65-70 (baada ya kuzaliwa kwake Yesu), pengine kwa njia ya kukatwa vipande viwili, au kwa kusulubishwa huko Uingereza. Lakini tamaduni zingine zinasema kwamba Simoni aliuawa kwa sababu ya imani yake huko Uajemi, wakiwa pamoja na Thadayo.

Simoni Mzelote anakumbukwa kama mtu aliyejitolea mhanga kwa mafundisho ya Yesu na pia kwa kukua kwa kanisa la kwanza. Hata ingawa yeye alikuwa mmoja wa mitume ambao hawakujulikana sana, ukakamavu wake na kujitolea kwake kwa uenezaji wa ujumbe wa Kristo ni ukumbusho wa jinsi wafuasi wa Yesu walikuwa na machimbuko ya aina tofauti tofauti, na pia kwamba wao walikuwa na motisha tofauti tofauti kama wafuasi wa Yesu. Maisha yake pia yanatuonyesha sisi sote taswira ya maisha ya mtu aliyegeuzwa na ambaye alikuwa amejitolea kwa ajili ya kuweko kwa amani na umoja. ■

Anwani


The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

Utakatifu kwa Bwana

# THADAYO (LEBAUSI, YUDA)

## MHIMIZAJI, MTAFUTAJI WA UKWELI MWENYE MAWAZO MENGI



Thadayo, ambaye pia anajulikana kama Yuda mwana wa Yakobo, alijulikana pia kama Lebausi. Msomi mmoja wa karne ya nne anayeitwa Yerome alimwita Thadayo "Mtu aliyekuwa na majina matatu." Jina lake linapatikana katika orodha ya mitume katika vitabu vya Injili; lakini jina lake mara nyingi huwa limefichika katikati ya majina ya wanafunzi wale wengine, na kwa hivyo hatuna habari nyingi kuhusiana na maisha yake. Inachukuliwa kwamba Thadayo alizaliwa Galilaya, mahali ambapo wengi wa mitume walizaliwa, hata ingawa habari kabambe kuhusiana na maisha yake ya mwanzoni haiko.

Katika Injili ya Yohana, Thadayo anatambulika kwa sababu ya kumuuliza Yesu swali mahususi wakati wa sherehe ya Meza ya Bwana. Ananukuliwa akimuuliza Bwana, "Bwana, imekuwaje ya kwamba wataka kujidhihirisha kwetu, wala si kwa ulimwengu?" (Yohana 14:22), jambo ambalo liliashiria shauku yake ya kutaka kuelewa utume wa Yesu na sifa za kiasili za huduma ya Yesu.

Baada ya kufufuka kwa Yesu, Thadayo alifanyika kuwa mhubiri shupavu wa imani ya Kikristo, na akashiriki katika uenezaji wa injili. Mapokezi ya Kanisa yanasema kwamba Thadayo alihubiri katika sehemu tofauti tofauti, ikiwemo Yudea, Samaria, Siria, Uajemi (Iran), na Armenia. Thadayo anachukuliwa kuwa aliwahubiria na kuwasaidia watu wengi wa Mataifa ili wapate wokovu, na anahusishwa na uanzilishi wa makundi ya mwanzo ya Kikristo katika sehemu hizo.

Habari tofauti za mapokezi kuhusu kifo cha Thadayo zinatofautiana, lakini taarifa nyingi zinasema kwamba yeye aliuawa kwa sababu ya imani kati ya miaka ya 65-80 (baada ya kuzaliwa kwake Yesu). Baadhi ya mapokezi yanasema kwamba yeye aliuawa huko Edessa (Uturuki), pengine kwa kupigwa rungu hadi kufa au kwa kupigwa mawe.

Wasomi wengine wanaamini kwamba Thadayo ndiye aliandika waraka wa Yuda, hata ingawa maoni yanayokubalika sana kuhusu kitabu hicho yasema kwamba kiliandikwa na Yuda mwingine, ambaye pengine alikuwa binamu au ndugu wa kambo wa Yesu. Hakuna jawabu kamili kuhusiana na swala hilo, kwa sababu pia kuna watu wanaoshikilia dhana kwamba Thadayo alikuwa na uhusiano wa kidamu na Yesu. Liwe liwalo, Thadayo anatambulika kuwa mfano wa maisha ya mtu aliyekuwa na imani na hata kujitolea, hata ingawa yeye hakutambulika sana kati ya kundi la mitume. ■